

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Nukushi: 0282501200
Barua pepe: aczl@ardhi.go.tz



Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Mkoa wa Mwanza,
S.L.P 668,
Mwanza.

Tafadhali unapojibu taja:

Kumb.Na. LD/LZ/74976/17

09.11.2020

Meneja Wa Kanda,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P 638,
Mwanza.

**YAH: KUWASILISHA FOMU YA ARDHI NA. 1 KWA AJILI YA KUTANGAZA ARDHI
INAYOKUSUDIWA KUTUMIKA KWA LENGU LA UWEKEZAJI**

Husika na kichwa cha Habari hapo juu.

Viwanja Na. 46 & 48 kitalu "V" Usagara Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi Vimeombwa na Kampuni ya HONGLIN INTERNATIONAL TRADE DEVELOPMENT CO. LIMITED ya S.L.P 6482 Mwanza, kwa ajili ya uwekezaji wa ujenzi wa kiwanda. Wamiliki wa Kampuni hii wenye hisa nyingi, ni raia wa kigeni.

Hivyo, utaratibu wa utoaji milki ya viwanja hivi, ni lazima itolewe kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Aidha, madhumuni ya matumizi ya ardhi husika, ni kwa ajili ya uwekezaji. Kwa mantiki hii, Kamishna wa Ardhi ameandaa Fomu ya Ardhi Na. 1 kwa ajili ya kutangaza ardhi tajwa inakusudiwa kutolewa milki kwa ajili ya uwekezaji.

Tunawasilisha fomu husika kwa ajili ya hatua zako stahiki za kusaini na kutangaza katika Gazeti la Serikali.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi
Kny: Kamishna wa Ardhi Msaidizi

Nakala:
Kamishna wa Ardhi,
S.L.P 2908,
Dodoma.

Honglin Interanational Trader Development Co. Limited, ..
S.L.P 6482,
Mwanza.